**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA**

**Unapojibu tafadhali taja:** **08 Januari, 2026**

**Kumb.Na. UA.12/261/01/13**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya Kufanya Kazi katika Halmashauri ya Jiji la Tanga Kuomba nafasi za Kazi ya Ualimu Katika Shule za Mchepuo wa Kiingereza (English Medium).

**1.0 WALIMU ( Nafasi 30)**
**(a) SIFA ZA KUAJIRIWA**

Awe mwenye Stashahada (Diploma) au Shahada ya Ualimu/Elimu yenye somo moja la Kufundishia au zaidi kutoka Katika Chuo Kinachotambuliwa na Serikali.

Kazi na Mjukumu:-

i. Kuandaa Azimio la Kazi, Maandalio ya Masomo, Nukuu za masomo na Mpango wa kazi wa Majukumu mengine aliyokabidhiwa.
ii. Kutengeneza na Kufaraghua zana za Kufundishia na Kujifunzia.
iii. Kufundisha, Kufanya Tathmini na Kutunza Kumbukumbu za Maendeleo ya Wanafunzi.
iv. Kusimamia na kufuatilia Mahudhurio ya wanafunzi Shuleni na Darasani.
v. Kusimamia malezi ya Wanafunzi kiakili, kimwili, kiroho na Kutoa Ushauri nasaha na Unasihi
vi. Kutoa Ushauri wa Kitaalamu na Kitaaluma Kuhusu Maendeleo ya Elimu
vii. Kusimamia Utunzaji wa vifaaa na Mali za shule
viii. Kufanya kazi nyingine utakazopangiwa na Mkuu wa Shule kulingana na majukumu ya shule

Maombi yote yatumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **15 Januari, 2026** saa **9:30 Alasiri.**

Maombi yatumwe kwa:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji la Tanga,
S.L.P. 178
**TANGA**.

**Tangazo hili linafuta tangazo la kazi lililotolewa tarehe 06 Januari, 2026.**

Limetolewa Na:-

Eng. Juma Hamsini
**MKURUGENZI WA JIJI**

Tanga Jiji, Barabara ya Hassani Ngwilizi,S.L.P 178 Tanga, Simu: +27 2643068, +27 2644530/3.
Nukushi: +255 27 2644141/272647905.Tovuti:info@tangacc.go.tz. Tovuti:www.tangacc.go.tz